**TANZANIA BASKETBALL FEDERATION**




# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA SHIRIKISHO LA MPIRA WA KIKAPU KWA KIPINDI CHA MIAKA MIWILI KUANZIA MWAKA 2022-2023

@tzbball



# YALIYOMO


*SURA YA KWANZA*

| | | |
|---|---|---|
| 1.1 | Kuhusu Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania | 1 |
| 1.2 | Dira | 1 |
| 1.3 | Dhima | 1 |
| 1.4 | Muundo wa Dhirikisho | 2 |
| 1.5 | Majukumu ya Shirikisho | 2 |

*SURA YA PILI*

| | | |
|---|---|---|
| 2.0 | Mapitio ya Utekelezaji wa Majukumu ya Shirikisho la Mpira wa Kikapu Kwa Kipindi cha Miaka Miwili | 4 |
| 2.1 | Utekelezaji wa Maagizo ya Bodi | 4 |
| 2.2 | Tathmini ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kamisheni za Shirikisho | 4 |

*SURA YA TATU*

| | | |
|---|---|---|
| 3.0 | Ushiriki Wa Mashindano ya Kitaifa na Kimataifa kuanzia 2022-2023 | 15 |
| 3.1 | Mashindano ya Kitaifa | 15 |

*SURA YA NNE*

| | | |
|---|---|---|
| 4.0 | Maendeleo ya Jumla Kwenye Mchezo wa Mpira wa Kikapu Pamoja na Changamoto Mbalimbali. | 22 |
| 4.1 | Premium Project Basketball Academy | 22 |
| 4.2 | FIBA Connected Stadium | 22 |
| 4.3 | Uzinduzi wa Jezi za Timu ya Taifa ya Mpira wa Kikapu | 22 |

*SURA YA TANO*

| | | |
|---|---|---|
| 5.0 | Hesabu Zilizokaguliwa za Shirikisho Kwa Mwaka 2022 | 25 |
| 4.1 | Hitimisho | 25 |

*Vambatanisho* 26


MINI
BASKETBALL

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Kuhusu Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania

Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF) ndilo Shirikisho pekee Rasmi la Mpira wa Kikapu lililopewa mamlaka na Serikali ya kusimamia, kukuza, kushiriki na kuendeleza Mpira wa Kikapu nchini. TBF imesajiliwa rasmi chini ya Sheria ya Baraza la Michezo la Taifa la Tanzania Julai 28, 2004. TBF inasimamia na kufanya kazi kwa karibu na Vyama vya Mikoa 26 ambavyo majukumu yake makuu ni kusimamia na kuendeleza programu za mpira wa kikapu pamoja na Ligi za Kikapu za Mikoa. Pia, TBF imeendelea kuhihimiza na kuhamasisha uundwaji wa Vilabu endelevu vya Mpira wa Kikapu nchini kote na inaendelea kufanya kazi kwa pamoja na kujenga mahusiano imara na wadau mbalimbali wa Kitaifa na Kimataifa kwa madhumuni ya kujenga mazingira chanya ya kuendeleza mpira wa Kikapu hapa nchini.

Tangu ilipoanzishwa, TBF imepata mafanikio mengi na maendeleo makubwa katika nyanja zote za mpira wa vikapu Kimataifa ikiwa pamoja na kuandaa Mashindano mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa ya Mpira wa Kikapu. Aidha, TBF imeendelea kuwa mwanachama mshiriki wa Shirikisho la Kimataifa la Vyama vya Mpira wa Kikapu Duniani (FIBA).

### 1.2 Dira


Dira yetu ni kuwa mchezo wa mpira wa kikapu unaimarishwa na kutambulika kama mchezo unaopendwa na wengi nchini Tanzania.

### 1.3 Dhima

Dhima yetu ni kuweka na kuonyesha utawala bora kupitia muundo wa kitaasisi wenye wajibu wa kutekeleza majukumu yaliyo kasimiwa kwa lengo
la kukuza mpira wa kikapu kupitia mchakato wa ushirikishwaji, mafanikio na ubora.



### 1.4 Muundo wa Shirikisho




### 1.5 Majukumu ya Shirikisho

Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF) linatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Katiba ya Shirikisho, Sheria na miongozo mbalimbali ya michezo pamoja na Mpango Mkakati wa Shirikisho. Majukumu hayo ni:-

i. Kuongoza, kusimamia na kuratibu shughuli zote za mpira wa kikapu nchini.
ii. Kudhibiti na kusimamia uteuzi wa walimu, waamuzi na wakufunzi wa mpira wa kikapu.
iii. Kukuza na kuendeleza maeneo yote ya ufanisi yanayohusiana na mpira wa kikapu kwa kushirikiana na mikoa yote.
iv. Kushirikiana na mikoa katika kuratibu, kusimamia na kuendeleza shughuli zote za mpira wa kikapu zinazo fanyika katika maeneo yao.

v. Kuratibu shughuli zote zinaohusu usajili na kuhama kwa wachezaji katika klabu za ndani na nje ya nchi.
vi. Kuandaa na kusimamia ushiriki wa timu za Tanzania kwenye michezo ya kimataifa.
vii. Kuunda na kuandaa timu za taifa za mpira wa kikapu.
viii. Kubuni, kukuza, kuendeleza na kutekeleza programu za kiufundi na maendeleo yao.
ix. Kusimamia ustawi wa vilabu, wilaya, mikoa na vyama vishiriki katika maendeleo yao.
x. Kuwa na mpango wa kupata viwanja na vifaa vya mchezo huu vyenye viwango vya kimataifa.
xi. Kufanya jambo lolote muhimu kwa manufaa ya maendeleo ya mpira wa kikapu.
xii. Kuimarisha Mifumo ya fedha pamoja na ufuatiliaji na tathmini
xiii. Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkakati wa shirikisho;
xiv. Kuandaa Taarifa za utekelezaji za shirikisho zinazohusu uendeshaji wa shughuli za mpira wa kikapu na kuziwasilisha kwenye Bodi;
xv. Kupoke ana kujadili taarifa za utekelezaji wa shughuli za mikoa;
xvi. Kuratibu upatikanaji wa fedha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za shirikisho;
xvii. Kuandaa maoteo ya Bajeti ya shirikisho kwa mwaka wa fedha 2023/24; na
xviii. Kuratibu Mafunzo mbalimbali ya muda mfupi na muda mrefu kwa makocha na waamuzi wa mpira wa kikapu nchini.



# SURA YA PILI

## 2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA SHIRIKISHO LA MPIRA WA KIKAPU KWA KIPINDI CHA MIAKA MIWILI KUANZIA 2022-2023

### 2.1 Utekelezaji wa Maagizo ya Bodi

*Jedwali Na. 1* **Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati**

| Na | AGIZO | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 1. | Uwepo wa kanuni na taratibu za uendeshaji wa Shirikisho | Shirikisho limesha andaa rasimu 13 za kanuni na taratibu mbali mbali ambazo zimeambatanishwa. |
| 2. | Kufanya ukaguzi wa mahes-abu ya Shirikisho kwa kipindi kilichopita 2018-2021. | Mchakato wa Ukaguzi wa hesabu ulishindikana kutokana na ukosefu wa vielelezo vya kutosha na maombi husika yalikabidhiwa kwa Baraza la Michezo kwa ushauri nah atua zaidi. |

### 2.2 Tathmini ya Utekelezaji wa Majukumu ya Kamisheni za Shirikisho

Ibara ya 21 ya Katiba ya Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF) imeelekeza kuundwa kwa Kamisheni Nane zenye kusaidia kutekeleza majukumu ya Shirikisho katika Nyanja tofauti. Hivyo, katika kipindi cha miaka miwili ya utekelezaji wa majukumu ya Shirikisho, Kamisheni mbalimbali zimetekeleza majukumu yake kama ifutavyo: -

#### *2.2.1 Kamisheni ya Makocha*

Kamisheni ya Makocha ya Shirikisho imefanya kazi kubwa katika miaka miwili iliyopita kwa kutekeleza majukumu yaliyoelezwa kwenye Ibara ya 23 ya Katiba ya Shirikisho. Miongoni mwa majukumu hayo ni kuandaa mtaala wa kufundisha makocha wa mpira wa kikapu katika madaraja matatu: Daraja la Awali, Daraja la Kwanza Taifa, na Daraja la Pili Taifa. Madaraja haya hupewa kulingana na vigezo vya elimu, uzoefu, na ujuzi wa mpira wa kikapu.

Kamisheni ilifanikiwa kuteua wakufunzi wa ndani kama vile Kocha Frank Masumba, Delphinus Penesis, Bahati Mgunda, Robert Manyerere, Benson Nyasebwa, na Ashraf Harun. Hawa wamechangia kwa kiasi kikubwa katika kupeleka elimu ya ukocha kwenye mikoa na taasisi mbalimbali nchini, kulingana na mahitaji ya madaraja yaliyotajwa hapo awali.

Mikoa na taasisi zilizonufaika na mafunzo haya ni pamoja na Tanga, Dodoma, Mwanza, Iringa, Manyara, Kilimanjaro, Mbeya, na Dar-es-Salaam. Zaidi ya

makocha 100 wamepata mafunzo haya na wanasajiliwa katika mfumo wa TBF Map. Hii imewezekana kwa ushirikiano na vyama vya mikoa ya mpira wa kikapu na maafisa michezo wa mikoa, pamoja na Chama cha Makocha wa Mpira wa Kikapu Tanzania (TBCA).

Kamisheni pia imeweza kufanikisha kozi ya kimataifa ya FIBA LEVEL 1 chini ya FIBA, ambapo makocha 15 kutoka maeneo mbalimbali ya Tanzania bara na visiwani walishiriki. Hii ni sehemu ya juhudi za kamisheni katika kuendeleza ukocha na kuweka msingi imara kwa maendeleo ya mpira wa kikapu nchini.



### *2.2.2 Kamisheni ya Waamuzi*

Kamisheni ya Waamuzi wa Mpira wa Kikapu ilikuwa na malengo mawili muhimu kwa kipindi cha miaka miwili (2) iliyopita. Lengo la kwanza lilikuwa kutengeneza waamuzi wapya 200 katika Daraja la Kwanza Taifa. Lengo la pili lilikuwa kuwapanga waamuzi katika madaraja wanayostahili kulingana na mwongozo wa Shirikisho la Mpira wa Kikapu Duniani (FIBA), yaani Daraja la Kwanza, Daraja la Pili, na Daraja la Tatu ngazi ya Taifa.

Kamisheni ilipata mafanikio makubwa katika malengo yake yote mawili. Walifanikiwa kuzalisha waamuzi wapya 308, ambao ni zaidi ya malengo waliyokuwa wamejiwekea awali ya kutengeneza waamuzi 200. Aidha, walifanikiwa kupanga waamuzi katika Daraja la Kwanza ngazi ya Taifa kwa idadi ya 308 na Daraja la Pili ngazi ya Taifa kwa idadi ya 40. Zoezi la kupanga madaraja litaendelea mwaka 2024.





Hata hivyo, kamisheni ilikumbana na changamoto kubwa ya upatikanaji wa fedha katika baadhi ya mikoa kwa ajili ya kozi za mafunzo ya waamuzi. Hii imesababisha baadhi ya mikoa kutokuwa na uwezo wa kushiriki mafunzo hayo licha ya uhitaji mkubwa.

Kwa mapendekezo, kamisheni imeshauri Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF) kutafuta wahisani ambao wanaweza kusaidia mikoa ambayo inahitaji mafunzo lakini haina uwezo wa kifedha. Pia, TBF inaweza kupendekeza kuwezesha mafunzo kwa mikoa miwili kila mwaka ambayo haina uwezo wa kifedha wakutosha kwa kushirikiana na wahisani.

### *2.2.3 Kamisheni ya watoto Wadogo na Mashule*

Katika mwaka 2022, Kamisheni ya Vijana na Shule ilishiriki kikamilifu katika mashindano ya FIBA Zone V yaliyofanyika Kampala, Uganda, kwa timu za wavulana na wasichana za U18. Timu zote mbili zilifanikiwa kushika nafasi ya pili na kufuzu kwa mashindano ya Afrika yaliyofanyika Antananarivo, Madagascar mnamo Julai 2022. Timu ya wasichana ya Tanzania ilimaliza katika nafasi ya nane kwenye mashindano hayo, jambo lililoongeza uzoefu na kuonyesha uwezo wa vijana wetu katika mashindano ya kimataifa.

Kamisheni iliendelea na juhudi zake kwa kushiriki katika mashindano ya FIBA Zone V yaliyofanyika Kigali, Rwanda mwezi september 2022, kwa timu za wavulana na wasichana za U16. Timu ya wasichana ilifanikiwa kushika nafasi ya pili, ikionyesha ustadi na bidii yao katika mchezo huo. Ushiriki huu uliwapa vijana wetu fursa ya kushindana na kujifunza kutoka kwa wenzao wa kanda mbalimbali, hivyo kuboresha viwango vyao vya uchezaji na kuimarisha timu za taifa kwa siku zijazo.









Pia, mwaka 2023 Kamisheni iliandaa tukio kubwa la kanda kwa kushirikiana na FIBA Africa na Basketball for Good Initiative, lililojulikana kama FIBA Mini Basketball Festival. Tamasha hili lilifanyika jijini Dar es Salaam katika viwanja vya Don Bosco Oysterbay na liliwaleta pamoja zaidi ya watoto 350 wa kiume na wa kike wenye umri chini ya miaka 14 kutoka maeneo mbalimbali ya Tanzania. Tamasha hili lilikuwa na lengo la kukuza na kuendeleza vipaji vya watoto wadogo katika mpira wa kikapu, pamoja na kuwapa nafasi ya kufurahia na kujifunza mchezo huu katika mazingira ya furaha na ushirikiano.

### *2.2.4 Kamisheni ya Wanawake*

Ripoti inahusu maendeleo ya mchezo wa kikapu cha wanawake nchini, ikilenga kwenye malengo, maendeleo, changamoto, na njia za kusonga mbele. Lengo kuu limekuwa kuinua mchezo wa kikapu kupitia mashindano mbalimbali yaliyoandaliwa na wadau tofauti, hususan kwa kuadhimisha Siku ya Mwanamke

Duniani. Mashindano na mabonanza haya yamekuwa na mchango mkubwa katika kuhamasisha wanawake na wasichana kushiriki katika mchezo wa kikapu. Lengo ni kuongeza hamasa na ufahamu juu ya umuhimu wa michezo kwa afya na maendeleo ya kijamii. Hata hivyo, bado kuna changamoto za kuhakikisha mabonanza haya yanafikia maeneo yote nchini ili kuwawezesha wasichana wengi zaidi kushiriki.

Katika hatua za maendeleo, timu za wanawake zimeshiriki katika mashindano ya kimataifa ya Zone V, na pia watoto chini ya miaka 18 na 16 wamekuwa wakishiriki kwa kiwango kikubwa. Ushiriki huu umewawezesha wachezaji kupata uzoefu wa kimataifa, kuboresha ujuzi wao, na kuongeza ushindani. Hii ni hatua muhimu katika kukuza vipaji vya vijana na kuwaandaa kwa mashindano ya juu zaidi katika siku zijazo. Licha ya mafanikio haya, changamoto zinabaki katika upatikanaji wa rasilimali na vifaa vya kisasa kwa ajili ya mafunzo na maandalizi ya mashindano.





Njia za kusonga mbele ni pamoja na kuongeza ushiriki wa timu za wasichana katika mashindano ya Umitashumta na Umiseta, na kuendelea kutembelea kambi za wasichana kama iliyopo Monduli kwa ajili ya maandalizi ya mashindano ya kimataifa. Pia, kuongezeka kwa idadi ya makocha na waamuzi kutokana na kliniki zilizokuwa zikiendeshwa mikoani na kamisheni husika ni hatua nzuri. Mafanikio haya yote yamepelekea kupata nafasi ya kuwa mjumbe wa kamati ya ukanda wa tano (Zone V), jambo linaloonyesha maendeleo na kuimarika kwa mchezo wa kikapu nchini. Njia nyingine muhimu ni kuhakikisha programu hizi zinaendelezwa na kupanuliwa ili kufikia maeneo mengi zaidi na kuboresha miundombinu ya michezo.




*2.2.5 Kamisheni ya Mipango na Maendeleo*

Katika kamisheni ya mipango na maendeleo, Shirikisho limelenga kuboresha uongozi na uwezo wa kitaasisi katika ngazi zote za mchezo wa kikapu. Hatua muhimu zimejumuisha kupitia upya muundo wa katiba ya mpira wa kikapu nchini, kutoa mafunzo kwa wasimamizi wa michezo katika ngazi ya kitaifa, kanda na vilabu, na kuweka mwongozo wa uendeshaji wa mashindano ya mpira wa kikapu ifikapo mwaka 2022. Vilevile, mafunzo ya usimamizi wa fedha yamepangwa kwa ajili ya mikoa 26 ifikapo mwaka 2024 ili kuhakikisha usimamizi thabiti wa kifedha katika ngazi zote za mchezo.

Kuhusu maendeleo na uendelevu, Kamisheni imeweka kipaumbele katika kuboresha programu za maendeleo kwa vijana, wanawake na walemavu, na pia kuboresha mazingira ya michezo na miundombinu ya mpira wa kikapu. Mikakati ni pamoja na kuandaa mtaala wa msingi wa mafunzo ya mpira wa kikapu kwa shule za msingi na sekondari hadi ilipoka mwaka 2023, na kuendesha programu za mafunzo kwa makocha, wakufunzi na walezi mara mbili kwa mwaka katika kila mkoa. Aidha, Kamisheni bado inaendelea na mkakati wake wa kujenga viwanja vya mpira wa kikapu vya nje angalau katika kila kanda nchini ifikapo mwaka 2025.

Kwa upande wa uwekezaji, Kamisheni imejikita katika kuboresha uwekezaji zaidi katika mchezo na kuongeza ustahimilivu wa kifedha wa mpira wa kikapu pamoja na kukuza chapa na taswira ya mpira wa kikapu nchini. Malengo ni pamoja na

kupata angalau mikataba miwili ya udhamini kila mwaka, kuanzisha vyanzo vipya vya mapato angalau viwili kila mwaka, na kuendesha kampeni za uhamasishaji na matangazo kila mwaka. Kamisheni pia imeanzisha tovuti rasmi ya TBF na kufungua na kuboresha akaunti mbali mbali za mitandao ya kijamii iili kuongeza ufanisi wa mawasiliano na uhamasishaji kwa wadau wa mpira wa kikapu ndani na nje ya nchi.








### *2.2.6 Kamisheni ya Watu wenye Ulemavu*

Katika kipindi cha mwaka 2022, Kamisheni ya Mpira wa Kikapu kwa Watu Wenye Ulemavu imefanya jitihada kubwa za kuboresha uongozi na uwezo wa kitaasisi. Mafunzo maalum yalitolewa kwa wasimamizi wa michezo katika ngazi ya kitaifa na mikoa mbalimbali ili kuhakikisha usimamizi bora na ufanisi wa shughuli za mpira wa kikapu kwa watu wenye ulemavu. Pia, Kamisheni ilihakikishia kuwa mpango wake mkakati na taratibu za uendeshaji wa michezo zinalingana na mahitaji maalum ya wachezaji wenye ulemavu, hivyo kuongeza ushiriki wao katika mchezo huo.

Mwaka 2023 Kamisheni ilijikita zaidi katika maendeleo na upanuzi wa programu za mpira wa kikapu kwa watu wenye ulemavu. Kamisheni ilianzisha na kuendesha programu za mafunzo kwa makocha na wachezaji katika mikoa mbalimbali ili kuboresha ujuzi na uwezo wao. Vilevile, mashindano na mabonanza maalum kwa watu wenye ulemavu yaliandaliwa kwa kushirikiana na Chama cha kitaifa cha Mpira wa Kikapu kwa watu wenye ulemavu (TWBA), yakihusisha





timu kutoka nchi mbalimbali kwenye mashindano ya kanda yaliyofanyika nchini Tanzania ikiwa na lengo kuu la kutoa jukwaa kwa wachezaji wenye ulemavu kuonyesha vipaji vyao na kujifunza kutoka kwa wenzao.

Katika juhudi za kuongeza uwekezaji na kuonekana, TWBA kilifanikiwa kupata udhamini kwa ajili ya vifaa na miundombinu ya michezo, ikiwa ni pamoja na viti vya magurudumu maalum kwa ajili ya mpira wa kikapu. Aidha, kampeni za uhamasishaji kupitia mitandao ya kijamii na vyombo vya habari zilifanyika ili kuongeza ufahamu na ushiriki wa jamii katika mpira wa kikapu kwa watu wenye ulemavu. Hii iliwezesha kujenga mtandao mzuri wa wadau na washirika ambao wameonyesha nia ya kusaidia na kushiriki katika maendeleo ya mpira wa kikapu kwa watu wenye ulemavu nchini Tanzania.

### *2.2.7 Kamisheni ya Tiba ya Michezo*




Katika mwaka 2022, Kamisheni ya Michezo na Tiba ilifanya semina maalum ya kimataifa ikijumuisha madaktari 33 wanawake kutokea nchi mbali mbali zilizo ukanda wa tano wa shirikisho la mpira wakikapu barani Afrika (FIBA Africa Zone V) ambazo zilikuwa Kenya, Sudani Kusini, Uganda, Rwanda, Burundi, Ethiopia, Eritrea, Somalia na wenyeji Tanzania iliyofanyika mnamo Septemba 2022 jijini Dar es Salaam, katika hoteli ya Travertine. Semina hii ililenga kuboresha ujuzi na maarifa ya madaktari wanawake katika masuala ya tiba ya michezo, hususan katika mpira wa kikapu. Watoa mada walijumuisha wataalam wa afya ya michezo waliotoa mafunzo kuhusu mbinu za kisasa za matibabu na jinsi ya kushughulikia majeraha yanayotokea wakati wa michezo. Semina hii ilikuwa na mafanikio makubwa na ilihudhuriwa na madaktari kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania.

Mwaka 2023, Kamisheni ilichukua jukumu kubwa la kuhakikisha wachezaji wa timu ya taifa wanakaguliwa kiafya kabla ya kushiriki kwenye mashindano ya FIBA Afrocan yaliyofanyika Mei 2023 katika Uwanja wa Ndani wa Taifa, Tanzania.

Kamisheni ilihakikisha kuwa wachezaji wote walipimwa ili kuthibitisha hali yao ya afya na utimamu wa mwili, hatua iliyosaidia kubaini na kushughulikia matatizo ya kiafya kabla ya mashindano. Utaratibu huu wa uchunguzi wa kiafya ulifanya iwezekane kwa wachezaji kushiriki mashindano wakiwa na afya njema na utimamu wa mwili.

Katika juhudi za kuongeza ufanisi na utunzaji wa afya za wachezaji, Kamisheni ilianzisha programu za mafunzo ya mara kwa mara kwa madaktari wa timu na watoa huduma za afya. Mafunzo haya yalihusisha mbinu bora za matibabu, kinga dhidi ya majeraha, na ushauri wa lishe bora kwa wachezaji.

Pia, Kamisheni imeendelea kushirikiana na hospitali na vituo vya afya ili kuhakikisha wachezaji wanapata huduma bora na za haraka wanapohitaji. Hatua hizi zote zimeimarisha afya na utimamu wa wachezaji, hivyo kuongeza ufanisi na mafanikio katika michezo ya mpira wa kikapu nchini Tanzania.

### *2.2.8 Kamisheni ya Ufundi na Uendeshaji wa Mashindano*

Kamisheni ya Ufundi na Mashindano ya TBF ndio kamisheni pekee inayosimamia na kuratibu shughuli zote za ufundi katika mpira wa kikapu nchini ikiwemo uandaaji wa kanuni za mashindano, viwanja, usimamizi wa vifaa vya shirikisho na uandikaji wa ripoti mbalimbali. Miongoni mwa mashindano yaliyosimamiwa na kamisheni hiyo kwa mwaka 2022/2023 ni pamoja na Robinson Cup, Nyerere Cup, Ligi ya Muungano, Shindano la Kanda ya Tano Afrika kwa Wanawake, Ligi ya Taifa kwa Vilabu (NBL), Shindano la CRDB Taifa Cup.

Katika kipindi hicho, kamisheni ilipokea malalamiko na kutatua migogoro ya usajili wa wachezaji kwenye mikoa ya Kigoma, Kilimanjaro na Mwanza. Pia, iligawa vifaa vya shirikisho ikiwemo mipira na vifaa vingine vya mashindano kwa baadhi ya mikoa. Zaidi ya hapo, kamisheni imesisitiza usajili wa wachezaji, makocha, walimu na madaktari kwenye mfumo wa TBF Map kama ilivyoelekezwa kwenye kanuni za mashindano. Kuhusu waamuzi, kamisheni inashauri wachaguliwe kutokana na utendaji wao uliokaguliwa na wakurugenzi wa mikoa husika.

Katika juhudi za kuendeleza ligi kuu ya kikapu nchini (NBL), kamisheni imetoa mapendekezo ya kuboresha utaratibu wa uendeshaji wake kwa kuanzisha ligi za mikoa (RBA) ambazo zitachezwa kwa miezi mitatu hadi kuvutoa timu zitakazocheza hatua za makundi, 16 bora, robo fainali, nusu fainali na fainali. Mapendekezo hayo yanalenga kuongeza idadi ya michezo, ubingwa wa wachezaji na waamuzi pamoja na kuvutia mashabiki zaidi. Hata hivyo, changamoto kubwa itakuwa upande wa gharama ambazo zinatarajiwa kugharamiwa na timu zenyewe kwa kiasi kikubwa.


PAZI
FIBA


JKT



# SURA YA TATU

## 3.0 USHIRIKI WA MASHINDANO YA KITAIFA NA KIMATAIFA

### 3.1 Mashindano ya Kitaifa

*3.1.1 Shindano la Mabingwa wa Mikoa (CRDB-Taifa Cup)*

Kwa kipindi cha mwaka 2022 na 2023 Shirikisho limefanikiwa kufanya Shindano la kimikoa lijulikanalo kama Taifa Cup ambapo kwa mwaka wa 2022 lilifanyika mkoani na kuhusisha jumla ya timu 36 kutoka mikoa mbali mbali Tanzania bara na visiwani (i.e. likiwa na jumla ya timu 20 za wanaume na timu 16 za wanawake) ambapo Bingwa wa Mwaka 2022 kwa upande wa wanaume na wanawake ulikuwa ni Mkoa wa Dar ES Salaam.



Hata hivyo kutokana na changamoto mbali mbali za kiutawala kwa upande wa wadhamini wa Shindano hili la Taifa Cup kwa mwaka 2023 halikuweza kufanyika kwa mujibu wa kalenda ya Shirikisho kwa mwaka 2023. Hilo lilichangiwa na muingiliano wa majukumu kwa upande wa mdhamini mkuu wa Shindano husika Benki ya CRDB na pia Kituo cha Matangazo ya televisheni cha Azam nacho kukosa ratiba ya kuonyesha mashindano hayo kwa kubanwa na ratiba ya michuano ya Afrika kwa Mpira wa Miguu (I.e. Africa Super League) iliyofanyika jijini Dar ES Salaam kipindi husika.

Hata hivyo mdhamini ameonyesha nia ya kuedelea kudhamini Shindano la Taifa Cup katika baadhi ya maeneo yanayohusu mchezo moja kwa moja kama Ufundi, Utawala, Vifaa, Jezi, Zawadi na Matangazo.

### 3.1.2 *Ligi ya Taifa ya Mpira wa Kikapu (NBL)*

Shirikisho limefanikiwa kufanya ligi yake ya Taifa ijulikanayo kama National Basketball League (NBL) kwa misimu miwili (i.e. 2022 na 2023) ambapo kwa mwaka wa 2022 Kilele cha hatua ya mtoa ya ligi ya taifa (i.e. NBL Playoffs) ilifanyika mkoani Dar ES Salaam na timu ya Pazi Basktball Club kufanikiwa kutwaa Ubingwa wa ligi ya taifa kwa upande wa wanaume na timu ya Vijana Queens kufanikiwa kutwaa ubingwa wa ligi ya Taifa kwa upande wa wanawake.




Timu ya Pazi na Vijana Queens zilifanikiwa kujikatia tiketi ya kuliwakilisha Taifa katika michuano ya kimataifa kwa ngazi ya vilabu ijulikanayo kama Basketball Africa league (BAL) kwa timu ya wanaume ya Pazi na Africa Women Basketball League (AWBL) kwa timu ya wanawake ya Vijana Queens na JKT Stars.

Kwa mwaka 2023 Bingwa wa taifa ilikuwa ni timu ya JKT Basketball Club kwa upande wa wanaume na Vijana Queens kwa upande wa wanawake. Timu hizo zilitangazwa kama mabingwa wapya wa mwaka 2023 wa ligi ya taifa ya mpira wa kikapu ngazi ya mtoano (i.e. NBL Playoffs) na hivyo timu ya JKT (wanaume) kufuzu kushiriki michuano ya kimataifa kwa vilabu ijulikanayo kama Basketball Africa league (BAL) kwa timu ya wanaume na Africa Women Basketball League (AWBL) kwa timu ya wanawake ya Vijana Queens na Fox Divas zilizofanikiwa kufika hatua ya fainali.




Pia kwa upande wa wanaume timu za Kisasa Heroes (Dodoma) na ABC (Dsm) zimefanikiwa kufuzu kucheza michuano mipya ya Ukanda wa Africa mashariki ijulikanayo kama East Africa Challenge Cup inayotarajiwa kufanyika mwaka 2024.

### *3.1.3 Mashindano ya Kimataifa*

Katika kipindi cha mwaka 2022 - 2023, Shirikisho limefanikiwa kushiriki katika mashindano mbali mbali ya kimataifa ikihusisha timu za taifa kwa vijana na wakubwa pamoja na vilabu kwa timu za kiume na kike.

### *3.1.4 FIBA AFRICA ZONE V-U18 (Boys and Girls) Preliminaries*




Timu zetu za Taifa za vijana walio chini ya miaka 18 kwa wavulana na wasichana zilishiriki mashindano ya kufuzu michuano ya Africa kwa nchi zilizo ukanda wa 5 wa Shirikisho la mpira wa kikapu barani Africa (i.e. FIBA Zone V) mweiz Juni , 2022 jijini Kampala, Uganda na kufanikiwa kushika nafasi ya pili.

### *3.1.4 FIBA AFRICA CHAMPIONSHIP (Girls)*



Timu ya Taifa ya vijana walio chini ya miaka 18 kwa wasichana ilifanikiwa kucheza Michuano ya Afrika kwa vijana walio chini ya miaka 18 nchini Madagascar mwezi Julai 2022 na kufanikiwa kushika nafasi ya nane baada ya kutolewa katika hatua ya robo fainali na wenyeji Madagascar. Hata hivyo Mchezaji Jeni Minja alifanikiwa kuchaguliwa kama mlinzi bora wa michuano hiyo.

### *3.1.5 FIBA AFROCAN (Men) Preliminaies*



Timu ya Taifa kwa wanaume ilifanikiwa kushiriki shindano la kufuzu michuano ya Afrika kwa wachezaji wanaocheza ligi za ndani ijilikanayo kama FIBA AfroCAN Qualifiers ambapo Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Michuano hiyo ambayo jumla ya timu 5 za wanaume zilishiriki ambazo ni Burundi, Rwanda, Eritrea, Sudani Kusini na wenyeji Tanzania. Ambapo Tanzania ilifanikiwa kushika nafasi ya 4.

### *3.1.6 FIBA AFRICA ZONE V U16 (Boys and Girls) Preliminaries*

Timu zetu za Taifa za vijana walio chini ya miaka 16 kwa wavulana na wasichana zilishiriki mashindano ya kufuzu michuano ya Africa kwa nchi zilizo ukanda wa 5 wa Shirikisho la mpira wa kikapu barani Africa (i.e. FIBA Zone V) yaliyofanyika jijini Kigali nchini Rwanda julai 2023 na timu ya wasichana kufanikiwa kushika nafasi ya pili.





### *3.1.7 FIBA AFRICA ZONE V-Women Championship*



Tanzania ilifanikiwa kuwa mwenyeji wa mashindano ya kimataifa kwa vilabu kwa timu za wanawake kwa nchi zilizo ukanda wa tano wa shirikisho la Mpira wa Kikapu Africa (i.e. FIBA Zone V) ambapo jumla ya timu 7 zilizshiriki kutoka mataifa mbali mbali (i.e. APR na REG kutoka Rwanda , Nile Sisters kutoka Sudan Kusini, KPA na Equity bank kutoka Kenya, Wolkite kutokana Ethiopia, Alexandria kutoka Egypt na wenyeji Vijana Queens kutoka Tanzania.

.

### *3.1.8 ROAD TO BAL Group C-Eastern Conference*





Timu ya Pazi ilifuzu kushiriki michuano ya awali ijulikanayo kama Road to BAL preliminaries iliyofanyika nchini Tanzania Oktoba 2023 na kufanikiwa kufuzu hatua ya 16 bora ambapo ilienda kucheza hatua ya mwisho kucheza kwenye fainali za michuano hiyo iliyofanyika katika jiji la Johanesburg, Afrika Kusini.





### *3.1.9 ROAD TO BAL Women Championship*

Timu za wanawake za Vijana Queens na JKT Stars zilifanikiwa kushiriki kwenye michuano ya awali ya Africa Women Basketball League kwa ngazi ya vilabu iliyofanyika nchini Rwanda November,2023. Hili lilikuwa ni toleo la kwanza la hili Shindano ambapo ilijumuisha jumla ya timu 8 kutokea nchi mbali mbali zilizo ukanda wa tano wa Shirikisho la Mpira wa Kikapu barani Afrika (i.e. FIBA Zone V) kama (i.e. Nile Sisters kutoka Sudan Kusini, KPA na Equity bank kutoka Kenya, Dynamo kutokana Burundi, Vijana Queens na JKT Stars kutokea tanzania na wenyeji APR na REG kutoka Rwanda.

# SURA YA NNE

## 4.0 MAENDELEO YA JUMLA KWENYE MCHEZO WA MPIRA WA KIKAPU PAMOJA NA CHANGAMOTO MBALIMBALI.

### A: Maendeleo ya Jumla

### 4.1 Premium Project Basketball Academy

Katika kuhakikisha kunakuwepo na miundombinu bora ya viwanja vya mpira wa kikapu nchini, Shirikisho la Mpira wa Kikapu (TBF) likishirikiana na Uongozi wa Manispaa ya Kigamboni lilifanikiwa kupewa eneo la Machava lililopo Kigamboni kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanja cha Mpira wa Kikapu. Hivyo, Shirikisho lilifanikiwa kumpata mdhamni wa ujenzi wa uwanja huo kutoka Premier Bet kupitia Premier Projects.

Hatua hii imefanikisha kuanzishwa kwa program ya kufundisha watoto wadogo zaidi ya 50 mchezo wa mpira wa kikapu (Primier Project Basketball Academy) pamoja na kuanzisha timu ya kike ya Mpira wa Kikapu ya Kigamboni Queens ambayo imeshiriki kwa mara ya Kwanza kwenye Ligi ya Mpira wa Kikapu Dar es Salaam. Pia kuna timu ya wavulana imeanzishwa inayoitwa Premier Project Boys amabyo inashiriki Development League (D-League)

### 4.2 FIBA Connected Stadium

Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania limefanya maombi kwa Shirikisho la Mpira wa Kikapu Duniani (FIBA) ili kujumuishwa kwenye Mpango wa FIBA na Synergy Sports wa kufunga mgumo wa kurekodi mchezo na matukio yote uwanjani pamoja na kuchakata data mbalimbali za Timu pamoja na wachezaji na mapitio ya waamuzi (FIBA Connected Stadium). Mfumo huu utafungwa kwenye viwanja vya ndani vya Mpira wa Kikapu vinavyotumika kwenye mashindano ya FIBA.

Nchi Kumi na Moja zimechaguliwa kuwa sehemu ya mpango ikiwemo Tanzania, na mpaka kukamilika kwake utagharimu Dola za Kimarekani 50,0000 sawa na shilingi milioni 120,000. Hivyo, mfumo huu utawezesha kuongeza ubora wa picha za matukio, utangazaji wa mchezo moja kwa moja, kutengeneza fursa za kibiashara pamoja na kushirikisha washabiki kupitia mitandao ya jamii.

### 4.3 Uzinduzi wa Jezi za Timu ya Taifa ya Mpira wa Kikapu

Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF) limefanya jitihada ya kutafuta mdhamini wa kutengenezea Jezi za Timu ya Taifa ya Wanaume na Wanawake. Katika jitihada hizo, shirikisho lilifanikiwa kupata Kampuni ya Michezo ya Kajumulo ambayo imetengeneza jezi za Timu ya Taifa ya Wanaume na Wanawake. Hivyo, shirikisho lilizindua Jezi hizo tarehe 04 Aprili 2024 Jijini Dodoma. Uzinduzi huo, umekuwa ni hatua muhimu kwa Shirikisho kuwa katika mstari wa mbele wa kukuza na kuendeleza mchezo wa mpira wa Kikapu nchini. Pia, inaashiria maono ya Watanzania mbalimbali waliopo nje wenye moyo wa uzalendo katika kuinua

viwango vya michezo ukiwemo mpira wa kikapu katika nchi yetu kupitia vifaa vya michezo na program mbalimbali za kuendeleza wachezaji na makocha wa mchezo wa mpira wa Kikapu. Kwa uungwaji huu wa mkono wa Kampuni ya vifaa vya michezo ya Kajumulo, timu yetu ya Taifa sio tu itaonekana kuwa sehemu bora, bali itajisikia kuwa na uwezo wa kuiwakilisha Tanzania kwa majigambo na dhamira kubwa katika medani ya kimataifa wakiwa nadhifu.

Jezi hizi si zaidi ya kitambaa na muundo wa nguo; bali zinabeba ndoto, matarajio, na bidii ya Wachezaji wetu wanaojitolea kwa mchezo wanaoupenda. Inaashiria umoja, ustahimilivu, na moyo usioyumba wa mpira wa kikapu wa Tanzania. Wachezaji wetu wanapovaa jezi hii, wamebeba matumaini na ndoto za Taifa letu, wakihamasisha vizazi vijavyo na kuacha urithi utakaodumu zaidi ya hadi vizazi vijavyo.



### B: Changamoto

Pamoja na mafaniko yaliyopatikana kwenye utekelezaji wa majukumu ya shirikisho na maendeleo ya ujumla, bado shirikisho linakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazokwamisha ukuaji wa kasi na maendeleo ya kikapu nchini

kama ifuatavyo:-

(i) Ugumu wa kupatikana kwa wafadhili. Shirikisho toka kuanzishwa kwake limekuwa likijitahidi kutafuta wafadhili kwa ajili ya kupata rasilimali fedha za kuendesha shughuli za shirikisho, mafunzo kwa program mbalimbali kwa makocha, waamuzi na wachezaji wa rika mbalimbali, kuandaa kambi na kusafirisha Timu za Taifa;

(ii) Miundombinu na vifaa. Bado kuna tatizo kubwa la uwepo wa miundombinu bora ya viwanja vya nje na ndani vya mpira wa kikapo pamoja na upatikanaji wa vifaa vya mchezo huu kwa gharama nafuu. Hali hii inadumaza maendeleo ya mchezo husika kwa wachezaji, makocha na wakufunzi pamoja na kukosa fursa za kuwa wenyeji wa mashindano makubwa ya kimataifa. Hata hivyo, TBF imekuwa ikiomba wadau mbalimbali kusaidia ujenzi wa viwanja kwenye baadhi ya maeneo ya mikoa mbalimbali pamoja na kupata misamaha ya kodi kwenye baadhi ya vifaa vya mchezo wa mpira wa kikapu nchini;

(iii) Kutokuwepo kwa Programu za msingi kwa vijana na Timu ya Taifa. Kutokana na kutokuwepo na rasilimali fedha ya uhakika kwa Shirikisho, kumekuwepo na ukosefu wa programu za msingi kwa vijana (U16-U18) za kutambua, kukuza na kuendeleza vipaji kwa vijana na hivyo kupelekea Timu zetu za Taifa kutokufanya vizuri kwenye mashindano ya Kimataifa;

(iv) Upatikanaji wa mafunzo mablimbali ya kimataifa. Eneo hili limekuwa ni changamoto kubwa kwa makocha na waamuzi hali inayopelekea kutokuwa na ujuzi endelevu kwa wahusika kulingana na mabadiliko mpira wa kikapu. Kwa nyakati tofauti, TBF imekuwa ikiomba na kupata msaada wa wakufunzi kutoka FIBA kwa lengo la kupunguza makali ya changamoto hii.

(v) Ushindani mdogo wa ligi za ndani. Kiwango cha ushindani na muonekano wa ligi za mikoa za mpira wa kikapo nchini bado kipo chini kwa baadhi ya mikoa na mikoa mingine haina Ligi kabisa. Hivyo, hali hii inazuia kasi ya maendeleo ya wachezaji, makocha na wakufunzi pamoja na umaarufu wa mchezo miongoni mwa mashabiki na wadau wa mpira wa kikapu;

(vi) Utangazaji wa mchezo kwenye vyombo vya habari. Bado kuna vyombo vichache vya habari vinavyojishughulisha moja kwa moja kwenye kutangaza mchezo wa mpira wa kikapu. Hali hii inapunguza muonekano na mvuto wa mpira wa kikapu na hivyo kuathiri ushiriki wa washabiki na mvuto wa kibiashara;

(vii) Utawala bora na uwajibikaji kwa viongozi. Bado kuna tatizo kubwa kwa baadhi ya viongozi wanaosimamia mchezo wa mpira wa Kikapu katika ngazi mbalimbali kutoweza kufuata sheria na taratibu za misingi ya uongozi na uwajibikaji katika maeneo yao ya kazi. Hali hii imekuwa ikileta migogoro isiyokuwa na tija katika maeneo yao ya kazi na hivyo kudumaza maendeleo ya mpira wa kikapu. Pamoja na uwepo wa changamoto hizi, Shirikisho limekuwa mstari wa mbele kuhakikisha sheria na taratibu za uongozi na uwajibikaji zinazingatiwa.

# SURA YA TANO

## 5.0 HESABU ZILIZOKAGULIWA ZA SHIRIKISHO KWA MWAKA 2022

Kulingana na shughuli mbali mbali zilizofanyika ndani ya kila mwaka. Shirikisho kwa kuzingatia katiba yake ibara ya 36 kifungu kidogo 36.5.5 mojawapo la jukumu la Kamati tendaji ni kuandaa na kupitia hesabu zinazotakiwa kufanyiwa ukaguzi kama yalivyo maelekezo ya Sheria ya baraza la michezo yanayompa msajili wa vyama vya michezo mamlaka ya kuwasilishiwa hesabu zilizo kaguliwa kwa kila chama chochote cha kitaifa au kimkoa.

Hivyo Shirikisho limeambatanisha taarifa kamili ya mkaguzi wa hesabu za Shirikisho kwa kipindi cha mwaka 2022-2023 kwa mapitio na mapokeo kabla ya kuwasilishwa Baraza la Michezo kama sheria inavyo elekeza.

## 5.1 HITIMISHO

Shirikisho linapenda kuwasilisha taarifa yake ya Utendaji kwa kipindi cha miaka miwili (i.e. 2022 na 2023) kwa mapokeo, mapitia na mapendekezo. hata hivyo Shirikisho linapenda kuikumbusha mikoa kuandaa taarifa zao za kiutendaji ambazo zinapaswa kuwa sehemu ya taarifa za kitaifa kwa wakati.

Aidh, Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF) linachukua nafasi hii kuishukuru Serikali kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ikiongozwa na Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro, Waziri Utamaduni, Sanaa na Michezo; Mhe. Hamis Mwinjuma, Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo; Ndugu Gerson Msigwa, Katibu Mkuu na Ndugu Dkt. Suleiman Serera, Naibu Katibu Mkuu kwa kutupatia ushirikiano wa kutosha na kutupa miongozo mbalimbali inayotuwezesha kusimamia, kukuza na kuendeleza mchezo wa kikapu nchini na hatimaye kuweza kukamilisha taarifa hii ya utekelezaji kwa kipindi cha Miaka miwili ya Uongozi wa Shirikisho.

Pia, Shirikisho linapenda kushukuru watendaji wote wa Baraza la Michezo Tanzania (BMT) likiongozwa na Katibu Mtendaji Ndugu Neema Msitha kwa kuwezesha na kutupa miongozo ya kusimamia majukumu ya Shirikisho kwa mujibu wa Sheria na Taratibu za kimichezo.

Mwisho, Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF) linaendelea kutimiza majukumu yake kwa kuunga mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuendeleza michezo nchini.

# VIAMBATANISHO

- Kanuni za Shirikisho
- Mpango kazi wa Shirikisho (Annual Action Plan)
- Mpango Mkakati wa Shirikisho

# SHIRIKISHO LA MPIRA WA KIKAPU TANZANIA

## KANUNI ZA MAADILI

TOLEO LA KWANZA

MACHI 2023

## Yaliyomo

**Utangulizi** .......... **29**
1. Heshima na Usawa .......... 29
2. Nidhamu na Uadilifu .......... 29
3. Uchezaji wa Haki .......... 29
4. Usalama na Afya .......... 29
5. Ustawi wa Wachezaji .......... 29
6. Kuepuka Migongano ya Maslahi .......... 29
7. Uaminifu na Uwazi .......... 30
8. Matumizi ya Vifaa na Rasilimali .......... 30
9. Kuheshimu Mazingira .......... 30
10. Matumizi ya Teknolojia na Mitandao ya Kijamii .......... 30
11. Malalamiko na Utoaji wa Habari .......... 30

# UTANGULIZI

Kanuni hizi za maadili zimeandaliwa ili kuhakikisha kuwa kila mshiriki wa Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF) anafuata viwango vya juu vya tabia na uadilifu. Kanuni hizi zitatumika kwa wachezaji, makocha, waamuzi, viongozi, na wadau wote wa mpira wa kikapu nchini Tanzania.

## 1. Heshima na Usawa

1.1. Kila mshiriki anatakiwa kuheshimu na kuthamini haki za kila mtu bila kujali rangi, jinsia, dini, kabila, au hali yoyote ya kijamii.

1.2. Ubaguzi wa aina yoyote hautavumiliwa.

## 2. Nidhamu na Uadilifu

2.1. Washiriki wote wanapaswa kuonyesha nidhamu ya hali ya juu katika kila kipengele cha mchezo.

2.2. Udanganyifu, rushwa, na vitendo vyovyote vya udanganyifu havitavumiliwa.

## 3. Uchezaji wa Haki

3.1. Wachezaji wanapaswa kucheza kwa kufuata sheria na kanuni za mchezo, bila kutumia mbinu za hila au madawa ya kuongeza nguvu.

3.2. Kila mshiriki anatakiwa kuheshimu maamuzi ya waamuzi na viongozi wa mchezo.

## 4. Usalama na Afya

4.1. Usalama na afya ya wachezaji ni kipaumbele. Kila mshiriki anatakiwa kuhakikisha mazingira salama ya kucheza na kufuata taratibu za afya na usalama.

4.2. Wachezaji wanatakiwa kufanya ukaguzi wa kiafya mara kwa mara ili kuhakikisha wako katika hali nzuri ya kiafya.

## 5. Ustawi wa Wachezaji

5.1. Kila mshiriki anatakiwa kuchangia katika ustawi wa wachezaji, hasa vijana, kwa kutoa mwongozo na msaada unaohitajika.

5.2. Ukatili wa aina yoyote, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji wa kijinsia, hauruhusiwi na lazima uripotiwe mara moja.

## 6. Kuepuka Migongano ya Maslahi

6.1. Kila mshiriki anapaswa kuepuka hali yoyote inayoweza kusababisha mgongano wa maslahi. Maamuzi yote yanapaswa kufanywa kwa manufaa ya mchezo na washiriki wake.

6.2. Wajibu wa uwazi na uwajibikaji katika masuala ya kifedha ni muhimu.

## 7. Uaminifu na Uwazi

7.1. Kila mshiriki anatakiwa kuwa mkweli na mwaminifu katika shughuli zote zinazohusiana na mpira wa kikapu.
7.2. Taarifa zote zinazohusiana na mchezo zinapaswa kuwa wazi na kupatikana kwa urahisi.

## 8. Matumizi ya Vifaa na Rasilimali

8.1. Vifaa na rasilimali za TBF vinapaswa kutumika kwa uangalifu na kwa malengo yaliyokusudiwa.
8.2. Ubadhirifu wa mali za TBF hautavumiliwa.

## 9. Kuheshimu Mazingira

9.1. Kila mshiriki anatakiwa kuheshimu na kulinda mazingira katika maeneo ya michezo.
9.2. Usafi na utunzaji wa viwanja na vifaa vya michezo ni jukumu la kila mshiriki.

## 10. Matumizi ya Teknolojia na Mitandao ya Kijamii

10.1. Matumizi ya teknolojia na mitandao ya kijamii yanapaswa kuwa ya kuwajibika na ya kimaadili.
10.2. Uvunjaji wa faragha, kueneza habari za uongo, na lugha ya matusi havitavumiliwa.

## 11. Malalamiko na Utoaji wa Habari

11.1. Malalamiko yoyote yanapaswa kuwasilishwa kupitia njia rasmi zilizowekwa na TBF.
11.2. Kila mshiriki ana haki ya kutoa taarifa na malalamiko bila hofu ya kulipiziwa kisasi.


# HITIMISHO

Kwa kufuata kanuni hizi za maadili na miongozo mingine ya mchezo, Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania lina amini kuwa mchezo utaafanyika katika mazingira ya haki, usawa, na uadilifu katika kuendeleza mchezo wa mpira wa kikapu nchini Tanzania.

# Mpango kazi wa Shirikisho (Annual Action Plan)

TANZANIA BASKETBALL FEDERATION 2024 ANNUAL ACTIVITY PLAN

| ID | Task Name | Duration | Start | Finish |
|---|---|---|---|---|
| 1 | **1 TANZANIA BASKETBALL FEDERATION ANNUAL PLAN 2024** | **290 days** | **02/01/2024** | **10/02/2025** |
| 2 | **1.1 Kuimarisha na kusimamia Utawala bora na uwajibikaji** | **260 days** | **02/01/2024** | **30/12/2024** |
| 3 | **1.1.1 Kufuatilia idadi ya vyama vya mikoa vilivyokamilisha chaguzi na muundo uliokamilika** | **260 days** | **02/01/2024** | **30/12/2024** |
| 4 | 1.1.1.1 Kuorodhesha vyama ambavyo vinatakiwa kukamilisha ( | 60 days | 02/01/2024 | 25/03/2024 |
| 5 | 1.1.1.2 Kufuatilia vyama vya mikoa ambavyo vina uongozi katika muundo ulio kamilika | 100 days | 02/01/2024 | 30/12/2024 |
| 6 | **1.1.2 Idadi ya vilabu vilivyokamilisha chaguzi na muundo ulioka** | **60 days** | **02/01/2024** | **25/03/2024** |
| 7 | 1.1.2.1 Kuorodhesha vilabu ambavyo vinatakiwa kukamilisha c | 60 days | 02/01/2024 | 25/03/2024 |
| 8 | 1.1.2.2 Kufuatilia vilabu ambavyo vina uongozi katika muundo ulio kamilika | 60 days | 02/01/2024 | 25/03/2024 |
| 9 | | | | |
| 10 | **1.2 Kuimarisha na kusimamia nidhamu ya kazi na maadili ya uong** | **240 days** | **02/01/2024** | **02/12/2024** |
| 11 | 1.2.1 Kufuatilia mashauri ya kinidhamu na kuyafanyia kazi | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 |
| 12 | | | | |
| 13 | **1.3 Kuhakikisha uwepo wa wa ofisi na watumishi wa shirikisho.** | **120 days** | **05/02/2024** | **19/07/2024** |
| 14 | 1.3.1 Kufungua ofisi za shirikisho | 80 days | 05/02/2024 | 24/05/2024 |
| 15 | 1.3.2 Kuajiri watumishi wa shirikisho (secretary na messenger) | 40 days | 27/05/2024 | 19/07/2024 |
| 16 | | | | |
| 17 | **1.4 Kujenga uwezo kwa mikoa na vilabu** | **84 days** | **02/01/2024** | **26/04/2024** |
| 18 | 1.4.1 Kufuatilia mikoa ambayo haijasajiliwa | 60 days | 05/02/2024 | 26/04/2024 |
| 19 | 1.4.2 Kufuatilia vilabu vyote ambavyo havijasajiliwa | 60 days | 02/01/2024 | 25/03/2024 |
| 20 | 1.4.3 Kufuatilia kila mkoa/klabu inafungua akaunti ya benki. | 60 days | 05/02/2024 | 26/04/2024 |
| 21 | 1.4.4 Kuendesha kozi za kiutawala kwa mikoa/vilabu. | 4 days | 02/01/2024 | 05/01/2024 |
| 22 | | | | |
| 23 | **1.5 Kuhakikisha uwepo wa kanuni na taratibu zitakazo saidia ufanisi katika utendaji wa shirikisho** | **120 days** | **02/01/2024** | **17/06/2024** |
| 24 | **1.5.1 Kuandaa na kuzipitisha kanuni na taratibu za kuendesha na kusimamia shughuli za shirikisho kitaifa.** | **120 days** | **02/01/2024** | **17/06/2024** |
| 25 | 1.5.1.1 Disciplinary | 120 days | 02/01/2024 | 17/06/2024 |
| 26 | 1.5.1.2 Gift & Hospitability | 120 days | 02/01/2024 | 17/06/2024 |
| 27 | 1.5.1.3 Safe guarding | 120 days | 02/01/2024 | 17/06/2024 |




Page 1

TANZANIA BASKETBALL FEDERATION 2024 ANNUAL ACTIVITY PLAN

| ID | Task Name | Duration | Start | Finish | Half 1, 2024 / Half 2, 2024 |
|---|---|---|---|---|---|
| 28 | 1.5.1.4 Grievances | 120 days | 02/01/2024 | 17/06/2024 | SG |
| 29 | 1.5.1.5 Equality | 120 days | 02/01/2024 | 17/06/2024 | SG |
| 30 | 1.5.1.6 Recruitment | 120 days | 02/01/2024 | 17/06/2024 | SG |
| 31 | 1.5.1.7 Match Fixing | 120 days | 02/01/2024 | 17/06/2024 | SG |
| 32 | 1.5.1.8 Betting | 120 days | 02/01/2024 | 17/06/2024 | SG |
| 33 | 1.5.1.9 Fraud & Corruption | 0 days | 02/01/2024 | 02/01/2024 | 02/01 |
| 34 | 1.5.1.10 Data Protection | 120 days | 02/01/2024 | 17/06/2024 | SG |
| 35 | 1.5.1.11 Code of Conduct | 120 days | 02/01/2024 | 17/06/2024 | SG |
| 36 | 1.5.1.12 Financial Regulations | 0 days | 02/01/2024 | 02/01/2024 | 02/01 |
| 37 | 1.5.1.13 Procurement Guideliness | 0 days | 02/01/2024 | 02/01/2024 | 02/01 |
| 38 | | | | | |
| 39 | **1.6 Ujenzi wa miundombinu ya mpira wa kikapu (Ofisi na viwanja)** | **240 days** | **02/01/2024** | **02/12/2024** | |
| 40 | 1.6.1 Kukarabati viwanja vilivyopo | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | K.U |
| 41 | 1.6.2 Kujenga viwanja vyipa | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | K.U |
| 42 | 1.6.3 Kujenga Ofisi za Shirikisho | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | SG |
| 43 | | | | | |
| 44 | **1.7 Kufungua kanzidata ya wachezaji,makocha,waamuzi na viongo** | **40 days** | **02/01/2024** | **26/02/2024** | |
| 45 | 1.7.1 Kuweka taarifa za vilabu na wachezaji | 40 days | 02/01/2024 | 26/02/2024 | K.UFUNDI,K.WATOTO,K.WANAWAKE,K |
| 46 | 1.7.2 Kuweka taarifa za makocha | 40 days | 02/01/2024 | 26/02/2024 | K.MAKOCHA |
| 47 | 1.7.3 Kuweka taarifa za waamuzi | 40 days | 02/01/2024 | 26/02/2024 | K.WAAMUZI |
| 48 | 1.7.4 Kuweka taarifa za mikoa na viongozi wake | 40 days | 02/01/2024 | 26/02/2024 | DSG,K.MIPANGO |
| 49 | | | | | |
| 50 | **1.8 Kuweka utaratibu wa BIMA ya afya kwa wachezaji wa Timu za** | **30 days** | **05/02/2024** | **15/03/2024** | |
| 51 | 1.8.1 Kutafuta udhamini wa bima kwa ajili ya timu za taifa | 20 days | 05/02/2024 | 01/03/2024 | SG,K.TIBA |
| 52 | 1.8.2 Kukata bima za timu za taifa (watoto na wakubwa) | 10 days | 04/03/2024 | 15/03/2024 | SG,K.TIBA |
| 53 | | | | | |
| 54 | **1.9 kusimamia viwango na ubora katika mchezo.** | **266 days** | **05/02/2024** | **10/02/2025** | |
| 55 | **1.9.1 Kuandaa/kuboresha mwongozo wa kanuni za mashindano** | **266 days** | **05/02/2024** | **10/02/2025** | |
| 56 | 1.9.1.1 Mchezo wa 5x5 | 0 days | 05/02/2024 | 05/02/2024 | 05/02 |
| 57 | 1.9.1.2 Mchezo wa 3X3 | 0 days | 05/02/2024 | 05/02/2024 | 05/02 |
| 58 | 1.9.1.3 Mchezo wa kikapu kwa watu wenye ulemavu | 20 days | 05/02/2024 | 01/03/2024 | K.WALEMAVU |
| 59 | 1.9.2 Kuandaa makongamano/semina za kujenga uelewa wa kan | 20 days | 04/03/2024 | 29/03/2024 | K.MIPANGO,DSG |

Page 2

TANZANIA BASKETBALL FEDERATION 2024 ANNUAL ACTIVITY PLAN

| ID | Task Name | Duration | Start | Finish | Half 1, 2024 / Half 2, 2024 (J F M A M J J A S O N D) |
|---|---|---|---|---|---|
| 60 | | | | | |
| 61 | **1.10 Kujenga utamaduni wa kikapu.** | **240 days** | **02/01/2024** | **02/12/2024** | |
| 62 | **1.10.1 Kubuni mbinu mbali mbali za kusogeza mchezo karibu na** | **240 days** | **02/01/2024** | **02/12/2024** | |
| 63 | 1.10.1.1 CSR | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | M |
| 64 | 1.10.1.2 Makongamano ya kitaaluma | 4 days | 02/01/2024 | 05/01/2024 | K.MIPANGO,K.WATOTO |
| 65 | 1.10.1.3 Sanaa na Ubunifu katika mchezo | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | K.\ |
| 66 | | | | | |
| 67 | **1.11 Kuanzisha programu mbali mbali za kubadilishana uzoefu.** | **120 days** | **02/01/2024** | **17/06/2024** | |
| 68 | **1.11.1 Kutafuta programu mbali mbali za kubadilishana uzoefu** | **120 days** | **02/01/2024** | **17/06/2024** | |
| 69 | 1.11.1.1 Viongozi | 120 days | 02/01/2024 | 17/06/2024 | SG |
| 70 | 1.11.1.2 Makocha | 120 days | 02/01/2024 | 17/06/2024 | SG,K.MAKOCHA |
| 71 | 1.11.1.3 Waamuzi | 120 days | 02/01/2024 | 17/06/2024 | SG,K.WAAMUZI |
| 72 | 1.11.1.4 Wachezaji | 120 days | 02/01/2024 | 17/06/2024 | SG,K.MIPANGO |
| 73 | | | | | |
| 74 | **1.12 Kusimamia na kushiriki katika mashindano mbali mbali ya mpira wa kikapu** | **226 days** | **19/01/2024** | **29/11/2024** | |
| 75 | **1.12.1 Mashindano ya Kitaifa** | **184 days** | **04/03/2024** | **14/11/2024** | |
| 76 | 1.12.1.1 Ligi za mikoa | 80 days | 04/03/2024 | 21/06/2024 | K.UFUNDI,K.MIPANGO,K |
| 77 | 1.12.1.2 Ligi ya Taifa | 115 days | 06/05/2024 | 11/10/2024 | SG,K.UFU |
| 78 | 1.12.1.3 Taifa Cup | 10 days | 01/11/2024 | 14/11/2024 | DSG, |
| 79 | **1.12.2 Mashindano ya Kimataifa** | **226 days** | **19/01/2024** | **29/11/2024** | |
| 80 | 1.12.2.1 FIBA Afrobasket Men | 2 days | 19/01/2024 | 22/01/2024 | SG,DSG,K.WANAWAKE,K.MIPANGO,K.UFUN |
| 81 | 1.12.2.2 FIBA Women Champions Cup | 8 days | 20/11/2024 | 29/11/2024 | SG, |
| 82 | 1.12.2.3 ROAD TO BAL | 10 days | 18/11/2024 | 29/11/2024 | SG, |
| 83 | 1.12.2.4 FIBA U18 Qualifiers | 10 days | 10/06/2024 | 21/06/2024 | SG,DSG,K.WATOTO,K.M |
| 84 | | | | | |
| 85 | **1.13 Kubuni njia mbali mbali za kuongeza vyanzo vya mapato kwa shirikisho.** | **240 days** | **02/01/2024** | **02/12/2024** | |
| 86 | 1.13.1 Kuingia mikataba ya udhamini/ufadhili | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | PR |
| 87 | 1.13.2 Kuandaa programu mbali mbali za maendeleo ya mchezo | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | K.I |
| 88 | 1.13.3 Kupokea ruzuku toka serikalini kendeleza mchezo. | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | PR |

Page 3

TANZANIA BASKETBALL FEDERATION 2024 ANNUAL ACTIVITY PLAN

| ID | Task Name | Duration | Start | Finish | Half 1, 2024 / Half 2, 2024 (J F M A M J J A S O N D) |
|---|---|---|---|---|---|
| 89 | **1.13.4 Kukusanya mapato yatokanayo na huduma mbali mbali zinazotolewa kupitia mchezo** | **240 days** | **02/01/2024** | **02/12/2024** | |
| 90 | 1.13.4.1 Mauzo ya biadhaa zitokanazo na nembo, rasilimali zingine zitokanazo na mchezo. (i.e. apparels, items, etc.) | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | M. |
| 91 | 1.13.4.2 Mapato yatokanayo na matangazo kwa njia ya kimtandao kupitia mitandao ya kijamii. | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | M. |
| 92 | 1.13.4.3 Mapato yatokanayo na ada za ushiriki mashindano mbali mbali ya kitaifa | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | M. |
| 93 | 1.13.4.4 Mapato yatokanayo na leseni za wachezaji , makocha, waamuzi na wadau wengine wa mchezo. | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | M. |
| 94 | 1.13.4.5 Mapato yatokanayo na ada za kuendesha mashindano mbali mbali ya kitaifa/kimataifa | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | M. |
| 95 | | | | | |
| 96 | **1.14 Kusimamia na kuratibu uandaaji wa mpango wa bajeti na matumizi bora ya fedha za shirikisho.** | **261 days** | **02/01/2024** | **31/12/2024** | |
| 97 | 1.14.1 Kuandaa,kupitisha na kutumia bajeti na matumizi ya shirik | 40 days | 02/01/2024 | 26/02/2024 | PRESIDENT,SG,M.HAZINA |
| 98 | 1.14.2 Kutoa mafunzo ya njia bora za kuandaa mahesabu na kutoa ripoti zake kwa mikoa. | 10 days | 27/02/2024 | 11/03/2024 | PRESIDENT,M.HAZINA |
| 99 | 1.14.3 Kusimamia vyama vya mikoa kutunza hesabu zao | 20 days | 12/03/2024 | 08/04/2024 | SG,M.HAZINA |
| 100 | 1.14.4 Kusimamia mchakato wa kupatikana ripoti ya ukaguzi ya Fedha za Shirikisho | 60 days | 09/04/2024 | 01/07/2024 | SG,M.HAZINA |
| 101 | 1.14.5 Kuandaa ripoti za fedha kwa kila robo ya mwaka | 261 days | 02/01/2024 | 31/12/2024 | |
| 102 | | | | | |
| 103 | **1.15 Kupanua wigo wa ushirikiano na wadau katika kukuza mchezo kupitia programu mbali mbali.** | **240 days** | **02/01/2024** | **02/12/2024** | |
| 104 | **1.15.1 Kuandaa mikataba ya ushirikiano wa kimkakati na wadau mbali mbali** | **240 days** | **02/01/2024** | **02/12/2024** | |
| 105 | 1.15.1.1 Vyuo na taasisi za elimu | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | PR |
| 106 | 1.15.1.2 Makampuni | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | PR |
| 107 | 1.15.1.3 Mawakala wa ndani na nje | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | PR |
| 108 | 1.15.1.4 Vituo vya michezo | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | PR |
| 109 | 1.15.1.5 Taasisi za kijamii | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | PR |
| 110 | 1.15.1.6 Taasisi za Serikali | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | PR |

Page 4

TANZANIA BASKETBALL FEDERATION 2024 ANNUAL ACTIVITY PLAN

| ID | Task Name | Duration | Start | Finish | Half 1, 2024 / Half 2, 2024 (J F M A M J J A S O N D) |
|---|---|---|---|---|---|
| 111 | 1.15.1.7 Taasisi za kimataifa | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | PR |
| 112 | | | | | |
| 113 | **1.16 Kuboresha mahusiano kati ya shirikisho na wadau (i.e. serikali , vyama vya kitaalamu, taasisi na makampuni).** | **240 days** | **02/01/2024** | **02/12/2024** | |
| 114 | **1.16.1 Kujenga mahusiano ya kiutendaji na wadau** | **240 days** | **02/01/2024** | **02/12/2024** | |
| 115 | 1.16.1.1 Serikali (BMT na Wizara) | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | PR |
| 116 | 1.16.1.2 Vyama vya kitaalamu | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | PR |
| 117 | 1.16.1.3 Taasisi | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | PR |
| 118 | 1.16.1.4 Makampuni | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | PR |
| 119 | | | | | |
| 120 | **1.17 Kuimarisha na kuendeleza mahusiano ya Shirikisho kimkoa, kitaifa, kikanda na kidunia** | **0 days** | **02/01/2024** | **02/01/2024** | 02/01 |
| 121 | **1.17.1 Kujenga mahusiano ya kiutendaji na wadau** | **0 days** | **02/01/2024** | **02/01/2024** | 02/01 |
| 122 | 1.17.1.1 FIBA International | 0 days | 02/01/2024 | 02/01/2024 | 02/01 |
| 123 | 1.17.1.2 FIBA Africa | 0 days | 02/01/2024 | 02/01/2024 | 02/01 |
| 124 | 1.17.1.3 FIBA Zone V | 0 days | 02/01/2024 | 02/01/2024 | 02/01 |
| 125 | 1.17.1.4 Mikoa | 0 days | 02/01/2024 | 02/01/2024 | 02/01 |
| 126 | | | | | |
| 127 | **1.18 Kukuza na kuendeleza mahusiano kati ya Shirikisho na Serikali pamoja na taasisi zake** | **240 days** | **02/01/2024** | **02/12/2024** | |
| 128 | 1.18.1 Kufanyia kazi maelekezo na miongozo toka (BMT/Wizara) | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | SG |
| 129 | 1.18.2 Kufanya programmu za pamoja kati ya Shirikisho na Serikali (BMT/Wizara) | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | PR |
| 130 | | | | | |
| 131 | | | | | |
| 132 | **1.19 Kutumia utalii wa kimichezo kama njia ya mapato na kutangaza nchi na mchezo.** | **240 days** | **02/01/2024** | **02/12/2024** | |
| 133 | 1.19.1 Kubuni huduma mbali mbali kwa kushirikiana na taasisi za | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | SG |
| 134 | | | | | |
| 135 | **1.20 Kuanzisha kitengo cha habari na mahusiano** | **22 days** | **02/01/2024** | **31/01/2024** | |
| 136 | 1.20.1 Kupata afisa habari wa Shirikisho | 0 days | 02/01/2024 | 02/01/2024 | 02/01 |
| 137 | 1.20.2 Kuandaa majukumu na mpango kazi wa kitengo | 22 days | 02/01/2024 | 31/01/2024 | K.MIPANGO |

Page 5

TANZANIA BASKETBALL FEDERATION 2024 ANNUAL ACTIVITY PLAN

| ID | Task Name | Duration | Start | Finish | Half 1, 2024 / Half 2, 2024 (J F M A M J J A S O N D) |
|---|---|---|---|---|---|
| 138 | | | | | |
| 139 | **1.21 Kusimamia na kuendeleza program mbalimbali za timu za tai** | **22 days** | **02/01/2024** | **31/01/2024** | |
| 140 | 1.21.1 Kuteua mkurugenzi wa ufundi wa programu ya maendeleo ya timu za taifa | 0 days | 02/01/2024 | 02/01/2024 | **02/01** |
| 141 | 1.21.2 Kuandaa na kusimamia mpango wa maendeleo ya timu ya | 15 days | 08/01/2024 | 26/01/2024 | **K.MIPANGO,K. MAKOCHA,K.WATOTO,K.WA** |
| 142 | 1.21.3 Kuteua kamati maalum ya timu za taifa | 3 days | 29/01/2024 | 31/01/2024 | **PRESIDENT,VP,SG** |
| 143 | | | | | |
| 144 | **1.22 Kuanzisha mafunzo kwa walimu katika mashule (i.e. msingi na sekondari).** | **249 days** | **02/01/2024** | **13/12/2024** | |
| 145 | 1.22.1 Kutoa mafunzo ya ngazi mbalimbali za ukocha | 215 days | 19/02/2024 | 13/12/2024 | **K** |
| 146 | 1.22.2 Kutoa mafunzo ya ngazi mbalimbali za uamuzi | 215 days | 19/02/2024 | 13/12/2024 | **K** |
| 147 | 1.22.3 Kutoa mafunzo ya afya na usalama michezo katika ngazi m | 215 days | 19/02/2024 | 13/12/2024 | **K** |
| 148 | 1.22.4 Kufuatilia ujenzi /upatikanaji wa miundo mbinu ya mchezo katika mashule na maeneo ya kijamii | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | **K.l** |
| 149 | 1.22.5 Kuingia makubaliano ya kutoa mafunzo ya mchezo kwa walimu/wanafunzi kupitia chuo cha michezo Malya. | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | **PR** |
| 150 | | | | | |
| 151 | **1.23 Kuanzisha programu za maendeleo ya wachezaji.** | **240 days** | **02/01/2024** | **02/12/2024** | |
| 152 | **1.23.1 Kuwezesha uanzishwaji wa programu mbalimbali za maendeleo ya wachezaji** | **240 days** | **02/01/2024** | **02/12/2024** | |
| 153 | 1.23.1.1 Watoto | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | **K.** |
| 154 | 1.23.1.2 Wanawake | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | **K.** |
| 155 | 1.23.1.3 Watu wenye ulemamvu | 240 days | 02/01/2024 | 02/12/2024 | **K.** |

# Mpango Mkakati wa Shirikisho

## STRATEGIC PLAN 2021 – 2025

**TANZANIA BASKETBALL FEDERATION**

Our **VISION** is that Basketball is well established and recognized as a sport of choice across Tanzania with the **MISSION** to establish and demonstrate good governance through an organizational structure, with defined roles and responsibilities, mandated to maximize the growth of Basketball through a process of participation, achievement and excellence.

**Our Values**
Respect , Dedication, Professionalism , Teamwork , Integrity

| | GOVERNANCE | SUSTAINABILITY | DEVELOPMENT | INVESTMENT | VISIBILITY |
|---|---|---|---|---|---|
| KEY RESULTS AREAS | Enhance leadership and institutional capacity at all levels of the game. | Improve financial sustainability and investment portfolio. | Enhance development programmes for youth, women and disabled. | Enhance basketball infrastructure and playing environment. | Promote Tanzania basketball's brand and image. |
| STRATEGIC OBJECTIVES | • Revise constitutional structure of basketball in the country.<br>• Engage sport administrators trainings at national ,regional and club levels.<br>• Conduct regular compliance , audit and financial due diligence checks.<br>• Build standard basketball operational procedures for the sport administration. | • Build financial ethics and management capacity to regional associations.<br>• Establish Standardized financial structures across the basketball framework.<br>• Secure sponsorships for Basketball development programmes and events.<br>• Establish income generating activities/avenues to support basketball activities. | • Develop basketball fundamental training curriculum for primary & secondary schools.<br>• Enhance training programmes for coaches, trainers and Care takers.<br>• Develop and execute events calendar for the Youth, Women and Disabled.<br>• Provide Capacity Building workshops and seminars for the Youth, Women and Disabled | • Increase the number of basketball facilities (i.e. equipment's and courts).<br>• Established well organized nationwide events programmes.<br>• Enhance more training programmes for coaches , referees and other technical officials.<br>• Establish more collaborations with other stakeholders to positively engage the sport. | • Enhance relationships with other basketball stakeholders.<br>• Enhance effective use social media channels and other media outlets.<br>• Promote local & international tournaments.<br>• Increase basketball awareness activities for visibility.<br>• Engage social and welfare basketball activities. |
| MEASURES AND TARGETS | • New TBF constitution set in place by 2022<br>• Train at least 20 sport administrators every year.<br>• Set Basketball operating procedures in place by 2022. | • Train 26 regions on financial management by 2023<br>• Operationalize financial guidelines and procedures by 2023 on all regions.<br>• Secure at least 2 sponsorship deals every year.<br>• Establish at least 3 formal investments by 2024<br>• Collection of at least 15 Million Shillings annually.<br>• Increase at least 2 income sources annually. | • Endorse basketball fundamental training curriculum for secondary schools by 2022<br>• Develop strategy for National Team programme (NTP) by 2022.<br>• Conduct at least 2 training programmes for Coaches, Trainers and Care takers on every region twice a year.<br>• Organize and participate in at least 2 events for the Youth, Women and Disabled every year.<br>• Organize at least 2 life skills and empowerment seminars. | • Building at least 3 standard outdoor basketball courts in every zone across the country by 2025.<br>• Organize at least 4 major events every year.<br>• Train at least 10 coaches every region and every year.<br>• Train at least 10 referees every region and every year. | • Establish at least 5 long term working stakeholders MoUs by 2023.<br>• Establish and operationalize Official TBF Website, Social Media Channels, and working with other media partners by 2022.<br>• Establish awareness and promotion campaigns every year.<br>• Establish at least 2 corporate activities annually<br>• Establish at least 2 community programmes to link Basketball with community annually |

**TANZANIA BASKETBALL FEDERATION**

National Indoor Stadium | P.O Box 42089 Dar Es Salaam
TEL: +255 713 705 463 | +255 655 759 097 | info@tbf.or.tz
www.tbf.or.tz